



JAMHURI YA MUUNGANO WA
TANZANIA

TUME YA HAKI ZA BINADAMU
NA UTAWALA BORA



Juni 13, 2023

TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

Tamko la THBUB wakati wa maadhimisho ya Siku ya Kimataifa ya Uelewa Kuhusu Ualbino Juni 13, 2023

LEO Juni 13, 2023, Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora (THBUB) inaungana na wadau wote duniani kuadhimisha **Siku ya Kimataifa ya Uelewa Kuhusu Ualbino –“*International Albinism Awareness Day.*”**

Siku hii ilipitishwa na Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa kwa Azimio Na. A/HRC/RES/23/13 la Desemba 18, 2014 na ilianza kuadhimishwa rasmi mwaka 2015. Tangu wakati huo, kila ifikapo tarehe 13 Juni Dunia imekuwa ikiadhimisha siku hii ya Uelewa Kuhusu Ualbino.

Lengo kuu la kuwepo kwa siku hii ni kuhamasisha jamii kuhusu masuala mbalimbali ya Watu wenye Ualbino, ikiwemo kuwatambua na kutatua changamoto zinazowakabili.

Maadhimisho ya mwaka huu ni ya 18 kitaifa, na ya tisa (9) kimataifa, yenye Kauli mbiu ya Dunia: *“Ujumuishi ni Uimara (Inclusion is Strength).”* Kitaifa kauli mbiu ya mwaka huu ni: ***Tokomeza Saratani ya Ngozi kufikia Haki, Utu na Ustawi wa Watu wenye Ualbino;*** inayoangazia changamoto ya ugonjwa wa saratani ya ngozi unaowakabili Watu wenye Ualbino.

TUME YA HAKI ZA BINADAMU NA UTAWALA BORA

Ploti Na. 339, Mtaa wa Nyerere – Kilimani, S.L.P 1049, DODOMA/Ploti Na. 201, Mtaa wa Mbweni, S.L.P 285, ZANZIBAR

Simu: +255 734 047 775/734 119 978 (Makao Makuu); +255 (24) 2230494 (Zanzibar)

Barua Pepe: info@chragg.go.tz.zanzibar@chragg.go.tz; Tovuti: www.chragg.go.tz

THBUB inatumia siku hii kutambua na kupongeza jitihada za Serikali zote mbili, yaani Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Zanzibar kuhusu kulinda haki za Watu wenye Ualbino nchini. Aidha, Tume inawapongeza wananchi kwa ujumla katika kuendelea kukataa vitendo vya ubaguzi, unyanyapaa, ukatili na mauaji vitokanavyo na imani potofu na uelewa mdogo kuhusu ualbino katika jamii.

Hata hivyo, jitihada zaidi zinahitajika ili kuondoa kabisa changamoto za Watu wenye Ualbino hususan ugonjwa wa saratani ya ngozi; kwa kufanya hivyo kutawezesha ujumuishi wenye uimara wa kufurahia haki za binadamu kama zilivyoielezwa katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984, na Sheria za Watu Wenye Ulemavu ya Tanzania Bara na Zanzibar ambazo zinasisitiza utu wa mtu kuheshimiwa.

Hivyo basi, katika maadhimisho haya THBUB inapendekeza yafuatayo kwa wadau mbalimbali:

i) Serikali

- a) Kupitia Wizara zenye dhamana kwa Watu wenye Ualbino ziendeleo na juhudi za kuwatambua Watu wenye Ualbino na mahitaji yao, hususan kwa kutoa kinga na tiba ya saratani ya ngozi na kuweka mazingira mazuri kupitia mfumo wa utoaji wa huduma za afya nchini.

- b) Kupitia vyombo vyake vya ulinzi na usalama iendeleo kufanya ukaguzi wa mara kwa mara katika maeneo mbalimbali ili kuzuia na kuchukua hatua juu ya vitendo vya unyanyasaji dhidi ya Watu wenye Ualbino.

ii) Wananchi

- a) Watoe taarifa katika mamlaka husika juu ya vitendo vya udhalilishaji na unyanyasaji dhidi ya Watu wenye Ualbino katika maeneo yao;

b) Waachane na imani, mila, desturi na mitazamo potofu ambayo huwafanya Watu wenye Ualbino kujiona hawakubaliki, hawawezi na hawana mchango kwa jamii inayowazunguka na Taifa kwa ujumla katika shughuli zinazohusu maendeleo.

iii) Watu wenye Ualbino

Wazingatie miongozo ya afya juu ya kujikinga na saratani ya ngozi, pia wachukue hatua za haraka kwa kwenda hospitali pale wanapohisi wana vidonda vyovyote kwenye miili yao.

iv) Wadau wote

Waunganishe nguvu kutokomeza saratani ya ngozi kwa Watu wenye Ualbino ikiwemo kuendelea kutoa elimu kwa jamii juu ya kupinga vitendo vyote vya udhalilishaji, unyanyasaji na mauaji ya Watu wenye Ualbino.

Mwisho, Tume itaendelea kushirikiana na wadau wote katika kuhakikisha haki za Watu wenye Ualbino zinalindwa, zinakuzwa na kutetewa nchini.

“Ujumuishi ni Uimara (Inclusion is Strength).” “Tokomeza Saratani ya Ngozi kufikia Haki, Utu na Ustawi wa Watu wenye Ualbino.”

Imetolewa na:



Mathew P. M. Mwaimu (Jaji Mstaafu)
Mwenyekiti

TUME YA HAKI ZA BINADAMU NA UTAWALA BORA

Juni 13, 2023